JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI
SHULE YA SEKONDARI MWIKA

MAWASILAIONO
0755 536 499 **- MKUU** WA SHULE
0752 677 258 MAKAM MKUU WA SHULE
0754 237858 MAKAMU MKUU WA SHULE
0764 070 424 MWL. WA MALEZI
mwikasecondary@gmail.com
damiangwaltu@gmail.com

S. L. P 1945
MOSHI.

KUMB. NA. MWSS/JOIN/VOL – 2/2021

TAREHE:……

JINA LA MWANAFUNZI
…….....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWIKA - WILAYA YA MOSHI FORM (V) MWAKA 2021/2022

1.0 Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha **TANO** katika shule ya sekondari Mwika. Shule hii ipo umbali wa kilomita 43 kutoka Moshi Mjini barabara ya Moshi-Rombo. Kutoka Mwika sokoni ipo mita 200 upande wa kaskazini mwa soko la Mwika. Usafiri wa NOAH kutoka MOSHi mjini unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi MOSHI. Pia Unaweza shuka NJIAPANDA ya HIMO na kupanda NOAH za kwenda TARAKEA kwa nauli ya sh: 1500/= Nauli ya MOSHI kwenda MWIKA ni TSH. 3000/=. Mwika stendi kuja shuleni usafiri wa bodaboda ni Tsh. 1000/=, au kwa mguu kama hauna mizigo.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza mwezi JULAI 2021 kama tangazo la serikali linavyoelekeza kwa wanafunzi wa Kidato Cha Tano siku na tarehe ya kuripoti. unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **05/07/2021.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2:1. SARE.

(a) Wavulana:-

I. Suruali mbili (2) za heshima zenye marinda mawili (2) rangi ya **kijani ya choroko**, suruali isibane miguu (yaani modo) iwe na turn up. Kitambaa kimeambatanishwa.
II. Mashati mawili (02) meupe ya mikono mirefu yasiyobana mwili yenye vishikizo vya kawaida
III. Tai ndefu na sweta inayofanana na kitambaa cha suruali. Pia aje na mkanda mweusi wa ngozi usio na bakoli kubwa.
IV. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu, soksi ndefu nyeusi “pair” 04 zisizo na mchanganyiko wa rangi yoyote.
V. Shuka mbili (02) **rangi ya bluu**, mto na foronya, taulo, toilet paper (10 pieces), mswaki, dawa ya meno, **mablanketi** 02 rangi ya kijivu ya kawaida yasiyo ya sufi ndoo moja kubwa ya lita 20 ya plastiki, na ndoo moja ndogo (lita 10),

VI. madaftari makubwa(07 Quire 3), kalamu, na vitabu vyake binafsi angalau kimoja kwa kila somo katika tahasusi yake.

VII. Samani za hisabati (mathematical set) na scientific calculator kwenye masomo ya hisabati.
VIII. Godoro la ukubwa wa F2 ½ x F6 x 4”
IX. Bukta 02 za michezo rangi ya bluu/ nyekundu, raba za michezo, Suruali 02 nyeusi (zisizo bana, zenye marinda mawili na turn up) kwa ajili ya kazi za nje na kushindia, t-shirt 02 bluu/nyekundu zisizo na maandishi, Track-suit pea moja (sweta na suruali yake) ya rangi ya bluu.
X. Karatasi (ream) mbili aina ya A4 moja kwa ajili ya mitihani na nyingine kwa ajili ya mazoezi na majaribio kwa miaka miwili.
XI. Tranka (Sanduku) ukubwa wa kati, dishi (contena) la chakula, kijiko, kikombe cha chai/uji.
XII. Hard broom/brashi ngumu ya kudekia 1, Squeezer 1, Fagio 1 za chelewa fupi na slasher 1
XIII. Slippers **(Ndala)** pea 1 ya kuogea.

NB.

I. Nguo za nyumbani ambazo hazijaorodheshwa humu haziruhusiwi kabisa shuleni.
II. Baadhi ya vifaa vilivyoorodheswa hapo juu, unaweza kuvipata katika duka la shule.
III. Ili kuepuka kuchanganya rangi za uniform unashauriwa uje ushone uniform Mwika kwani kuna mafundi wazuri katiak soko lilo jirani na shule.
IV. Uje ukiwa umevaa sare ya shule siku ya kuripoti shuleni.
V. Mwanafunzi atanyoa nywele mara mbili kwa kila mwezi.
VI. Mwanafunzi aje na picha nane **(passport size)** iwe na back ground ya blue awe amevaa shati jeupe.
VII. Kila mwanafunzi aje na result slip ya kidato cha nne.

(b) Wasichana:-

I. Sketi mbili (2) au zaidi za heshima zenye marinda box mawili (2) mbele na nyuma zenye urefu unaofikia kwenye kifundo cha mguu na zenye **rangi ya kijani ya choroko**. Kitambaa kimeambatanishwa.
II. Mashati mawili (02) meupe ya mikono mirefu yasiyobana mwili yenye vishikizo vya kawaida
III. Tai ndefu na sweta inayofanana na kitambaa cha sketi.
IV. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu, soksi ndefu nyeupe “pair” 04 au zaidi.
V. Shuka mbili (02) **rangi ya pinki nzito**, mto na foronya, taulo, toilet paper (10 pieces), mswaki, dawa ya meno, **mablanketi** 02 rangi ya kijivu ya kawaida yasiyo ya sufi, ndoo moja kubwa ya lita 20 ya plastiki, na ndoo moja ndogo(lita 10), madaftari makubwa 07 (Quire 3), kalamu, samani za hisabati (mathematical set),scientific calculator na vitabu vyake binafsi angalau kitabu kimoja kwa kila somo katika tahasusi anayosoma.
VI. Godoro la ukubwa wa F2 ½ x F6 x 4”

VII. Bukta 02 za michezo rangi ya bluu/ nyekundu, raba za michezo, Sketi 02 nyeusi zenye marinda box mbili, 01 nyuma na 01 mbele zinazofikia urefu wa kifundo cha miguu kwa ajili ya kazi za nje (Kushindia), t-shirt 02 bluu/nyekundu zisizo na maandishi, Track-suit pea moja (sweta na suruali yake) ya rangi nyeusi.

VIII. Karatasi (ream) mbili aina ya A4 moja kwa ajili ya mitihani na nyingine kwa ajili ya mazoezi na majaribio kwa miaka miwili.

IX. Tranka (Sanduku) ukubwa wa kati, dishi (contena) la chakula, kijiko, kikombe cha chai/uji.

X. Fagio fupi ya chelewa (1), Drier (Squeezer) (01), jembe kubwa na mpini, rake 1.

XI. Kila mwanafunzi aje na result slip ya kidato cha nne.

XII. Slippers(ndala) pea 1 ya kuogea

NB.

i. Nguo za nyumbani ambazo hazijaorodheshwa humu haziruhusiwi kabisa shuleni .

ii. Baadhi ya vifaa vilivyoorodheswa hapo juu, unaweza kuvipata katika duka la shule.

iii. Ili kuepuka kuchanganya rangi za uniform unashauriwa uje ushone uniform Mwika kwani kuna mafundi wazuri katiaka soko lilo jirani na shule).

iv. Mwanafunzi atanyoa nywele mara mbili kwa kila mwezi.

v. Uje ukiwa umevaa sare ya shule siku ya kuripoti shuleni.

vi. Wasichana hawataruhusiwa kusuka nywele wakati wote wakiwa shuleni. Wakati wote wawapo shuleni nywele zinatakiwa kuwa fupi chini ya sentimita moja.

2:2 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

3:1: Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na marekebisho yake ya 2002 na **2009**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia **mambo ya msingi** yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.

(b) Ni lazima wanafunzi kuhudhuria vipindi vya masomo darasani na nje ya darasa.

(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni **(preparation)** kwa wanafunzi wa bweni/hosteli.

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shuleni na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(i). Kutunza mali za shule kama vile samani, umeme na miundo mbinu ya shule kwa ujumla.

2:3: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. . Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
5. Kupigana na kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya uma
7. Kudharua Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
10. Kuchochea, kuongoza na kushiriki migomo au kuvuruga amani na usalama wa mali au watu shuleni.
11. Kukataa adhabu halali kwa makusudi
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi pamoja na redio, au kifaa chochote chenye uhusiano na simu (laini, betri, earphone, headphone, vocha na flash.External hard disk, laptop,ipad na kifaa chochote cha ki-electronic).
13. Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia nyumbani kwa mtumishi yeyote.
14. Mwanafunzi akikosa masomo kwa siku 21 kwa mfululizo bila sababu ya msingi na ushahidi atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.

2:4: MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUTEKELEZA WAKATI WA KUJIUNGA NA SHULE.

1) Medical Examination Form ijazwe na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii
itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule/Msaidizi mara utakaporipoti shuleni***.(ikiwa mwanao ana matatizo ya kiafya hakikisha umemjulisha mkuu wa shule au mwalimu wa malezi, hakutakuwa na chakula maalum kwa wanafuzi wenye matatizo ya kiafya***)

2) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika kufanya migomo,fujo na makosa ya jinai ijazwe hapa shuleni.

3) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule kama kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule, ijazwe.

4) Mwanafunzi akamilishe malipo yote yaliyo orodheshwa katika jedwali la malipo.

5) Mwanafunzi asije na simu kabisa shuleni kwa matumizi ya simu shuleni atumie namba tajwa hapo juu na si vinginevyo.

2:5: ADA NA MICHANGO YA SHULE.

NA	MALIPO		
		MUHULA WA KWANZA	**MUHULA WA PILI**
1.	ADA YA SHULE	35,000.00	35,000.00
2.	TAALUMA	15,000.00	10,000.00
3.	TAHADHARI	10,000	-
4.	UKARABATI	5,000	-
5.	MALIPO KWA WAFAYAKAZI	15,000.00	10,000
6.	MAFUTA YA KANGAVU(Generator)	10,000.00	10,000.00
7.	HUDUMA YA KWANZA	10,000	5,000.00
8.	KITAMBULISHO	6,000.00	-
	JUMLA-TSH	**106,000**	**70,000**
	JUMLA KUU	**176,000/=**	

NB: MALIPO YOTE YALIPWE BENKI , AKAUNTI YA SHULE NA. 40301100215 **NMB** KWA KUANDIKA JINA LA MWANAFUNZI NA KIDATO ANACHOSOMA AJE NA RISITI (BANK PAY – IN – SLIP) ANAPORIPOTI SHULENI. FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA SHULENI – REJEA WARAKA NO. 13 KWA ELIMU 2009**.**

KARIBU SANA MWIKA SEKONDARI.

.....
D.P.GWALTU
MKUU WA SHULE

Nakala:
Katibu Tawala(M)
Mkoa wa Kilimanjaro
S.L.P 3003,
MOSHI.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya wilaya ya Moshi,
S.L.P 3003,
MOSHI.

Mwenyekiti wa Bodi,
Shule ya Sekondari Mwika,
S.L.P 1945,
MOSHI.

FOMU YA UTII WA SHERIA NA TABIA NJEMA

Mimi ……(jina kamili) kidato cha……Mwaka ……. Ninatambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi.

Naahidi:-

(a) Kwamba nitatii na kuheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya monitor,viranja,walimu watumishi wote hadi mkuu wa shule.

(b) Kwamba nimezisoma nakuzielewa na kuzifuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

(c) Kwamba sitatoka nje ya shule wakati wa masomo labla tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali kutoka kwa mwalimu mwenye dhamana husika au mkuu wa shule mwenyewe.

(d) Kwamba kama nitashindwa kufanya yote hayo hapo juu, hatua kali zichukuliwe dhidi yangu ambapo ni pamoja na kusimamishwa masomo/ kufukuzwa shule.

Tarehe…….. ……..
Jina na sahihi ya mwanafunzi.

Tarehe…… ……
Jina na sahihi ya shahidi Mzazi/Mlezi.

Tarehe…… .....……
Sahihi ya Mkuu wa wa shule.

MEDICAI EXAMINATION:

To be completed by a Medical Officer in a Government Hospital of all new extracts to Mwika Secondary School.

students name.....

Age ……

1. AIDS test
   .....
2. Blood count(red and white).....
3. Urine examination.....
4. Stool examination.....
5. Syphilis test.....
6. T.B. test
   .....
7. Ear test
   .....
8. Eye test.....
9. Spleen
   .....
10. Abdomen.....
11. Addition information of any Physical, Mental, Hereditary or Infections disease
    .....
    .....
    .....
12. Treatment after examination
    .....
    .....

(Please state nature of treatment)

MEDICAL CERTIFICATE:

I certify that the above mentioned individual has been examined and found fit/unfit to pursue secondary education.

Signature .....

Designation .....

Station .....

Date.....

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI.

A: HABARI ZA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani)
   ……..
   .....
2. Tarehe ya kuzaliwa……
   Dini……Dhehebu……..
3. Mahali, Wilaya na Mkoa
   ulipozaliwa……..
4. Shule uliyohitimu darasa la kumi na mbili (F4)……
5. Masomo unayo pendelea (i)…….
   (ii)……(iii)…….
6. Kazi yoyote uliyowahi kufanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba
   n.k……
7. Mambo unayopendelea nje na masomo(kama michezo,ushonaji)
   (i)…… (ii)……..……
   (iii)……..
8. Ninadhibitisha kwamba habari zilizotolewa ni kweli na sahihi.
   Jina la mwanafunzi..... sahihi..... Tarehe.....

B. HABARI ZA MZAZI/MLEZI.

1. jina kamili la baba.....yupo hai/amefariki.
2. Kazi yake.....
3. Jina kamili la mama..... yupo hai/amefariki.
4. Kazi yake.....
5. Jina kamili la mlezi (iwapo mwanafunzi haishi na wazazi wake).....
6. Kazi ya mzazi/mlezi.....
7. Namba ya simu ya mzazi/mlezi.....
8. Anuani ya mzazi/mlezi.....
9. Mtoto anaishi na (i) Baba (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote (iv)mlezi (kata isiyohusika)
10. Taja ndugu WANNE wa karibu wanao ruhusiwa kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni.

	JINA	**SIMU**	**UHUSIANO**
1.			
2.			
3.			
4.			

11. Mimi ..... Mzazi/Mlezi wa.....
    Nathibitisha kuwa taarifa hizo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na shule ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

    Jina la Mzazi /
    Mlezi.....……Sahihi.....Tarehe.....

VITABU VYA ZIADA AMBAVYO UNAWEZA KUMPATIA MWANAO ANAPOKUJA **SHULE (SIO LAZIMA)**

1. English language
    - Ashel,N(2017) Advanced Level English Language Structure and Stylistics: A Practical Approach: Dar Es Salaam. APE
    - Ashel,N(2017) English language 1 : Dar Es Salaam. APE
2. History
    - Advanced Level History 5 and 6 by Oxford
    - Essentials in Advanced Level History Paper 2 By Saleh Yassin
3. KISWAHILI
    - Nadharia ya Fasihi by Masebo and Nyambari Nyangine
4. MATHEMATICS
    - S,I(2015). Advanced Mathematics for Advanced Secondary: Form 5 and 6 Student Book: Dar Es Salaam GDY Publications Co. Limited.
    - Chand's S. (2012) Mathematics for class XI, XII (Vol.1 – 2)@. Delhi Chand and Loy Ltd.
5. GEOGRAPHY
    - KAMILI 2 (2016) “Practical Geography Alive” KAMILI BOOKS & GENERAL SUPPLIES.
    - MSABILA D. T (2012) “A Comprehensive Approach Physical Geography for Secondary School”, BY NYAMBARI NYANGWINE PUBLISHERS, DAR ES SALAAM
    - MSABILA D.T (2003) “ An Integrated Regional Study on Human and Economic Geography Advanceed Level Paper 2”, NYAMBARI NYANGWINE PUBLISHERS, DAR ES SALAAM, TANZANIA.
6. GENERAL STUDIES
    - KAMILI (2017) “General Studies revised version” KAMILI BOOKS & GENERAL SUPPLIES.
7. ECONOMICS
    - MTAEBWA (2012) Advanced Level Basic Economics, Kampala: EAP

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI
SHULE YA SEKONDARI MWIKA

CHECK LIST

Date of reporting……..time of reporting ……..

Students name ……..combination/class ……..

O-level school ……

S/N	KIFAA	IDADI	ZILIZOPO	MAONI
1	Suruali /sketi na tai	02		
2	Shati.	02		
3	Sweta ya shule	02		
3	Tracksuit	01		
4	Tshrt za shamba dress	02		
5	Shuka	02		
6	Viatu vyeusi vya kamba	02		
7	Ream paper	02		
8	Ndoo kubwa	01		
9	Ndoo ndogo	01		
10	Jembe lenye mpini	01		
11	Fagio chelewa	02		
12	Nembo	03		
13	drier/squeezer	01		
14	blanket(kijivu)	02		
15	picha pps	04		
16	Soksi pair	04		
17	Shamba dress-suruali/sketi	02		
18	Godoro 2.5x6	01		
19	Vifaa vya chakula	01		
20	file folder	01		
21	Raba za michezo	01		
22	Daftari counter quire 2	07		
23	Hard broom	01		
24				

Nb : vifaa tajwa hapo juu pi unaweza pata duka la shule.

Karibu mwika sekondari

……..

Mkuu wa shule